COLORADO
Department of Labor and Employment

# Tangazo la Colorado kuhusu Haki za Afya ya Umma Kazini:
# LIKIZO INAYOLIPIWA, UFICHUAJI SIRI NA VIFAA VYA KUJIKINGA

*Ilisasishwa tarehe 14 Julai, 2023*

*inaweza kusasishwa mara kwa mara*

## SHERIA YA FAMILIA NA MAHALI BORA PA KAZI ("HFWA"): Haki za Likizo Inayolipiwa

**Uangaziaji: Waajiri wote wa Colorado, wa ukubwa wowote, lazima wawe na likizo inayolipiwa**

- Waajiriwa wote wanapata saa 1 ya likizo inayolipiwa kwa kila saa 30 za kufanya kazi ("ongezeko la likizo"), hadi saa 48 kwa mwaka.
- Waajiriwa wanahitajika kulipwa kiwango cha malipo cha kawaida wakati wa likizo na lazima mwajiri aendelee kuwapa fidia zao.
- Ongezeko la likizo isiyotumika la hadi saa 48 linahamishwa kwa matumizi ya mwaka unaofuata.
- Kwa maelezo kuhusu hali mahususi (saa zisizo za kawaida, malipo yasiyo ya saa, n.k.), soma Sheria ya Ulinzi wa Mishahara 3.5, 7 CCR 1103-7.
- Likizo ya kujaliza ya hadi saa 80 inatumika katika dharura ya afya ya umma (PHE), hadi wiki 4 baada ya PHE kukamilika.*

**Waajiriwa wanaweza kutumia ongezeko la likizo kwa mahitaji ya usalama au ya afya yanayofuata:**

(1) ugonjwa wa akili au mwili, jeraha, au maradhi ya afya yanayozuia kazi, ikiwemo utambuzi wa ugonjwa au huduma ya uzuiaji;

(2) dhuluma za nyumbani, unyanyasaji wa kingono au unyanyasaji wa uhalifu unaosababisha mahitaji ya afya, uhamisho, kisheria au huduma nyingine;

(3) utunzaji wa mwanafamilia anayepitia hali iliyoelezwa katika kategoria ya (1) au (2);

(4) mahitaji ya kuomboleza msiba, mahudhurio ya matanga/makumbusho, au kifedha/kisheria baada ya kifo cha mwanafamilia;

(5) kutokana na hali mbaya ya hewa, kukatika kwa nishati/joto/maji au tukio jingine lisilotarajiwa, mwajiriwa anahitaji (a) kuhama makazi yake, au (b) amtunze mwanafamilia ambaye shule au kituo cha utunzaji kilifungwa; *au*

(6) katika PHE, afisa wa umma alifunga mahali pa kazi, au shule au kituo cha utunzaji cha mtoto wa mwajiriwa.

**Sera za Mwajiri (Notisi; Rekodi; Ongezeko la Matumizi; Faragha; na Rekodi za Likizo Inayolipiwa)**

- **Notisi na matangazo yaliyoandikwa.** Lazima waajiri (1) wawape waajiriwa wapya bila kupitisha nyaraka/sera nyingine za kuajiri; na (2) waonyeshe matangazo yaliyosasishwa na kutoa notisi zilizosasishwa kwa waajiriwa wa sasa, kufikia mwisho wa mwaka.
- **Notisi ya likizo "inayotabirika".** Waajiri wanaweza kutumia "taratibu zinazofaa" kwa njia ya maandishi kuhusu jinsi waajiriwa wanavyopaswa kutoa notisi ikiwa wanahitaji likizo "inayotabirika", lakini **hawawezi kunyima likizo inayolipiwa** kwa kutotii sera hiyo.
- **Mwajiri anaweza kuhitaji rekodi ya kuonyesha kwamba ongezeko la likizo ilikuwa sababu ya kustahiki ikiwa tu likizo ilikuwa ya siku nne au zaidi za kazi mfululizo** (*yaani* siku ambazo mwajiriwa angekuwa amefanya kazi, si siku za kalenda).
- **Rekodi haihitajiki ili *kupata* ongezeko la likizo**, lakini inaweza kuhitajika pindi tu mwajiriwa anaporudi kazini au anapoondoka kazini (yoyote inayotangulia). **Hakuna rekodi inayoweza kuhitajika kwa likizo ya PHE.**
- **Ili kurekodi likizo kwa ajili ya mahitaji ya yanayohusiana na afya ya mwajiriwa (au ya mwanafamilia wa mwajiriwa)**, mwajiriwa anaweza kutoa: **(1)** waraaka kutoka kwa mtoa huduma wa afya au wa jamii *ikiwa* huduma zilipokelwa na waraka unaweza kupatikana wakati unaofaa na bila gharama ya ziada; ***vinginevyo* (2)** maandishi ya mwajiriwa binafsi.
- **Rekodi ya dhuluma za nyumbani, unyanyasaji wa kingono, au unyanyasaji wa uhalifu** unaweza kuwa waraka au maandishi (1) juu (mfano, mtoa huduma za kisheria a hifadhi) au (2) juu, au waraka wa kisheria (amri ya uzuiaji, ripoti ya posili, n.k.).
- **Ikiwa mwajiri anaona kuwa rekodi za mwajiriwa zina mapungufu,** lazima mwajiriwa: (A) amwarifu mwajiriwa ndani ya siku saba za kupokea rekodi au mwajiriwa kurudi kazini au kuondoka (yoyote inayotangulia), na (B) ampe mwajiriwa angalau siku saba za kushughulikia mapungufu.
- **Matumizi ya Ongezeko.** Kutegemea na sera ya mwajiri, waajiriwa wanaweza kutumia likizo kwa maongezeko ya saa au dakika sita.
- **Faragha ya Mwajiriwa.** Waajiri hawawezi kuwahitaji waajiriwa kufichua "maelezo" kuhusu taarifa za afya au usalama za mwajiriwa (au familia yake) zinazohusiana na HFWA; taarifa kama hizo lazima zichukuliwe kuwa rekodi ya siri ya matibabu.
- **Lazima rekodi zihifadhiwe na kutolewa wakati ombi limetumwa.** Lazima waajiri watoe rekodi ya kiasi cha sasa cha likizo inayolipiwa ambacho waajiriwa (1) wanacho kwa matumizi, na (2) tayari wametumia wakati wa mwaka wa sasa wa fidia, ikiwemo likizo yoyote ya PHF ya kujaliza. Taarifa zinaweza kuombwa mara moja kwa mwezi au wakati kuna haja ya likizo ya HFWA.

**Kisasi au Kuhitilafiana na Haki za HFWA**

- **Likizo inayolipiwa haiwezi kuchukuliwa kuwa "kutokuwepo"** kunakoweza kusababisha upigwaji kalamu au aina nyingine ya hatua mbaya.
- **Mwajiriwa hawezi kuhitajika kutafuta "mfanyakazi mwingine" wala fidia ya kazi wakati anaenda likizo inayolipiwa.**
- **Mwajiriwa hawezi kupiga kalamu, kutisha au kulipiza kisasi, au kuhitilafiana na utumiaji wa likizo na**, mwajiriwa ambaye: (1) anaomba au anaenda likizo ya HFWA; (2) anafahamisha au anamsaidia mtu mwingine kudai haki za HFWA; (3) anawasilisha malalamishi ya HFWA; au (4) anashirikiana/anasaidia katika uchunguzi wa ukiukaji wa HFWA.
- **Ikiwa malalamishi, ombi au shughuli nyingine ya mwajiriwa inayofaa na nia njema ya HFWA *si sahihi***, si lazima mwajiri akubali au kuiruhusu, lakini hawezi *kuchukua hatua dhidi ya* mwajiriwa kwa ajili hiyo. Waajiriwa *wanaweza* kukabiliwa na madhara ya kutumia vibaya likizo.

## USIMULIAJI NA UFICHUAJI SIRI YA AFYA/USALAMA UNAOLINDWA ("PHEW"):
### Haki za Wafanyakazi Kusimulia Matatizo ya Afya/Usalama Kazini na Matumizi ya Vifaa vya Kujikinga

**Uangaziaji: Waajiri na Waajiriwa Wote, Pamoja na Wakandarasi Fulani Huru**

- PHEW husimamia si tu "waajiri" na "waajiriwa," ila "**wakuu wote**" (mwajiri **au** biashara yenye angalau wakandarasi 5 huru) na "**wafanyakazi**" (waajiriwa **au** wakandarasi huru wanaofanyia kazi "mkuu").

**Haki za Wafanyakazi Kupinga Ukiukaji wa Afya/Usalama Kazini:**

- Ni kinyume cha sheria **kulipiza kisasi dhidi ya, au kuhitilafiana na,** hatua zifuatazo:
  (1) **kuibua matatizo yanayofaa**, ikiwemo njia isiyo rasmi, kwa mkuu, wafanyakazi wengine, serikali, au umma, kuhusu ukiukaji wa sheria za serikali za afya au usalama kazini, au tishio kubwa la afya au usalama kazini;
  (2) **kupinga *au* kutoa ushahidi, kusaidia, au kushiriki** katika uchunguzi au kesi kuhusu ulipizaji kisasi, au kuhitilafiana na mwenendo ulioorodheshwa hapo juu.
- Mkuu hahitaji kuangazia tatizo la mfanyakazi linalohusiana na PHEW, lakini bado hawezi kumpiga kalamu mfanyakazi wala kuchukua *hatua nyingine dhidi ya* mfanyakazi kwa ajli ya kuibua tatizo hilo, mradi tu tatizo liwe lilifaa na kwa nia njema.

**Haki za Wafanyakazi Kutumia Vifaa Vyao Binafsi vya Kujikinga ("PPE"):**

- Lazima mfanyakazi aruhusiwe **kuvaa kwa hiari PPE yake** (barakoa, kinga ya uso, glavu, n.k.) ikiwa PPE (1) inatoa **kinga zaidi** kuliko ile ya kazini, (2) **inapendekezwa** na shirika la afya la serikali (serikali kuu, jimbo au serikali za mitaa), na (3) haimfanyi mfanyakazi **kutoweza kufanya kazi**.

## HAKI ZA MALALAMISHI (chini ya HFWA na PHEW)

- Ripoti ukiukaji kwenye Kitengo kama malalamishi au taarifa za shughuli za udanganyifu bila kujitambulisha au kuwasilisha kesi katika mahakama baada ya kukamilisha njai za suluhu kabla ya kesi mahakamani.

Tangazo hili linatoa muhtasari wa sheria mbili za Colorado kuhusu afya ya umma kazini: C.R.S. § 8-13.3-401 et seq., (likizo inayolipiwa), na C.R.S. § 8-14.4-101 et seq. (ufichuaji siri bora na salama) ikiwemo marekebisho ya sasa kuanzia tarehe ya tangazo hili. Haiangazii sheria, kanuni wala amri nyingine za afya au usalama, ikiwemo chini ya Sheria ya serikali kuu ya Usalama na Afya ya Kikazi (OSHA), kutoka Idara ya Afya ya Umma na Mazingira ya Colorado (CDPHE), au kutoka mashirika ya afya ya umma ya serikali za mitaa. Wasiliana na mashirika hayo kwa taarifa hizo za afya na usalama.

*Katika **PHE**, waajiriwa wanapata saa za ziada za likizo kwa ajili ya kutoweza kufanya kazi, kupimwa, kuenda karantini, kutunza familia katika hali kama hizo na mahitaji husika. Hakuna PHE inayofanya kazi sasa; tangazo hili litasasishwa ikiwa itatangazwa.

**Lazima tangazo hili liwekwe mahali ambapo ni rahisi kwa wafanyakazi kufikia, lishirikiwe na wafanyakazi wa mbali, liwe katika lugha nyinginezo inavyohitajika na kubadilishwa kwa toleo lolote linalosasishwa kila mwaka.**

**Tangazo hili ni muhtasari na haliwezi kuaminika kuwa taarifa kamili ya sheria ya wafanyakazi. Kwa sheria, fomu za maelezo, tafsiri, maswali au malalamishi yote, wasiliana na:**

**KITENGO CHA VIWANGO NA TAKWIMU ZA WAFANYAKAZI, ColoradoLaborLaw.gov, cdle_labor_standards@state.co.us, 303-318-8441 / 888-390-7936.**